


Kugundua Historia ya Kilwa

Na vielelezo na Michael Sagikwa



Kitabu hiki kilifadhiliwa na Chuo Kikuu cha York chini
ya mpango wao wa Global Challenges Research Fund






KUGUNDUA HISTORIA YA KILWA

Kitabu hiki kiliandikwa na Stephanie Wynne-Jones na Jeffrey Fleisher, kwa usaidizi kutoka kwa Lyuba Vinogradova. Vielelezo ni Michael Sagikwa. Ufadhili wa uzalishaji wake ulitolewa na Mfuko wa Utafiti wa Changamoto za Ulimwenguni katika Chuo Kikuu cha York. Inatumia taarifa za uchimbaji wa Kilwa Kisiwani na Neville Chittick katika miaka ya 1960 na kazi za hivi karibuni zaidi za Stephanie Wynne-Jones na Jeffrey Fleisher huko Songo Mnara. Wazo la kitabu hicho lilitokana na Kamati ya Vijiji vya Magofu Songo Mnara, ikiwa ni sehemu ya mahojiano ya mradi wa Co-Production and Community Heritage in Tanzania (CONCH) unaofadhiliwa na Baraza la Utafiti wa Sanaa na Kibinadamu, Uingereza, na kuongozwa na Stephanie Wynne-Jones na Sara Perry.

Tunashukuru kwa mchango wa wakazi wa Kilwa na Songo Mnara katika hatua zote za kazi hii. Walikuwa muhimu kwa uchimbaji wote ambao umefanyika kwenye tovuti na ilikuwa nia yao katika matokeo ambayo yaliongoza kitabu hiki. Asante sana kwa wote waliohusika.



Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ni visiwa viwili, sehemu ya visiwa vidogo vilivyoko kando tu ya pwani katika wilaya ya Lindi, Tanzania. Vimekaa kati ya miamba tumbawe na mikoko. Ni makazi ya jamii zinazovua samaki katika miamba hiyo na kulima katika ardhi ya mandhari ya visiwa. Visiwa hivyo pia ni maarufu ulimwenguni kutokana na magofu yanayopatikana hapo: mabaki ya miji mikubwa yenye misikiti, kasri za kifalme na nyumba zilizojengwa kwa mawe tumbawe. UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni) limeiorodhesha miji ya Kilwa na Songo Mnara kuwa 'Urithi wa Dunia', ikimaanisha kuwa ni mifano bora ya ustaarabu wa Waswahili ambao unapaswa kulindwa na jumuiya ya kimataifa. ikimaanisha kuwa ni mifano bora ya ustaarabu wa Waswahili ambao unapaswa kulindwa na jumuiya ya kimataifa.




Lakini ni nini tunachokifahamu kuhusu Kilwa na Songo Mnara? Ni nini hadithi ya maeneo haya na tunaifahamuje? Je, yanaingiaje katika hadithi ya pwani ya Afrika Mashariki, au ya Waswahili? Majibu ya maswali haya yanatoka pande nyingi tofauti. Yanapatikana katika historia ambazo watu wa pwani wamerithisha, ambazo zinatupa hadithi za jinsi miji ilianzishwa na baadhi ya watu walioishi pale. Pia kuna vidokezo katika lugha ya Kiswahili yenyewe, kwani maneno na misemo inaweza kuonyesha uhusiano kati ya mahali na watu hapo zamani. Muhimu zaidi, maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara yamechunguzwa kwa njia ya akiolojia ambayo ni njia ya kufahamu yaliyopita kwa kuangalia mambo yaliyoachwa na watu wa kale. Akiolojia inayofanyika katika maeneo haya imekuwa muhimu sana kwa kutueleza kuhusu jamii zilizojenga na kuishi Kilwa. Pia imekuwa kiini cha hadithi ya pwani nzima ya Uswahilini na jinsi ustaarabu wa Waswahili ulivyoendelea katika miaka 1500 iliyopita.

Kilwa Kisiwani

Nyumba za kwanza ambazo zimeonekana katika eneo la Kilwa Kisiwani zilijengwa takriban miaka 1,100 iliyopita (276 Hijria/890 BK). Zilijengwa kwa udongo uliokandikwa juu ya kiunzi cha mbao. Labda zilifanana kidogo na nyumba za udongo leo, zenye umbo la mstatili na paa iliyotengenezwa kwa nyasi. Watu walioishi katika nyumba hizo walikuwa wakulima na wavuvi. Walilima na kula vyakula vya asili kama mtama na uwele, na kuvua samaki wengi na samakigamba kwenye miamba tumbawe. Walifuga mbuzi na ng'ombe, ingawa walikula nyama mara chache kwani pengine wanyama walikuwa wachache kuliko samaki. Nyama inaweza kuwa iliachwa kwa hafla maalum na sherehe.






Hatufahamu mengi sana kuhusu wakazi hawa wa awali wa Kilwa. Mabaki ya nyumba zao yameharibiwa na kufanywa kutoonekana na nyumba kubwa zaidi ambazo zilijengwa kwenye eneo moja katika miaka ya baadaye. Vifaa walivyotumia vinatuonyesha kuwa walifanya shughuli nyingi za ufundi. Vyombo vya udongo kutoka kwa nyumba hizi za awali vilitengenezwa mahali hapo na kisha kutumika kwa kuhifadhi chakula na kupikia. Moja ya mambo ya kuvutia kuhusu ufinyanzi huu ni kwamba umbo na mapambo yake ni sawa na vyungu vilivyotengenezwa kote katika pwani ya Tanzania na Kenya, na hata katika baadhi ya maeneo ya ndani kabisa ya nchi. Katika maeneo haya yote, watu walitengeneza na kutumia vyungu kwa umbo la mitungi mikubwa mipana. Huenda ilitumiwa kushiriki chakula kati ya familia au kikundi. Vyungu vimepambwa kwa miundo iliyokwaruzwa katika udongo mnyevunyevu; mara nyingi hii ni mistari iliyopishana, au maumbo ya pembetatu karibu na shingo ya mtungi. Ukweli kwamba watu katika maeneo haya yote walitengeneza vyungu sawa unaonyesha kwamba walitangana na pia kwamba walishiriki baadhi ya njia walizokula chakula. Ingawa inaonekana ajabu kwamba watu wanaoishi mbali sana wangetengeneza na kutumia vitu vile vile, kumbuka kwamba watu hao pia walizungumza lugha moja! Kandokando ya pwani yote wakati huu watu walizungumza aina ya awali ya Kiswahili (proto-Swahili) na hivyo tunajua kwamba walikuwa sehemu ya jamii moja na kwamba waliunganishwa kwa kila namna, pengine kupitia nchi kavu na pia bahari.



Pamoja na ufinyanzi, wenyeji wa awali wa Kilwa walitengeneza shanga kutoka kwa kombe na vitu vya chuma. Huenda walifuma mikeka ya nyasi na vikapu, au kutengeneza vitambaa vya pamba. Walifanya biashara na mabaharia waliotoka Ghuba ya Uajemi. Huko Kilwa, tunapata vipande vya mitungi mikubwa yenye mng'ao wa samawati, ambayo ilitengenezwa katika nchi ambayo sasa ni Iraki na ambayo ilitumiwa kwenye meli kubeba tende, mafuta na pengine divai. Meli hizo kisha zilisafiri kurudi nyumbani hadi Ghuba ya Uajemi baada ya kubadilisha shehena yao kwa bidhaa kutoka Kilwa. Hii yawezekana ilikuwa mbao za mikoko, ambari, chuma, pembe za ndovu au hata watumwa. Ni vigumu kujua. Tunachofahamu ni kwamba biashara ilikuwa sehemu ndogo sana ya maisha pale Kilwa katika kipindi hicho. Ni vipande vichache tu vya mitungi hii ya samawati vilivyopatikana katika mji, ikilinganishwa na maelfu mengi ya vipande vya ufinyanzi wa mahali pale.



Katika karne ya kumi na moja (kuanzia mnamo takriban 390 Hijria/1000 BK) mambo yalianza kubadilika pale Kilwa. Mji ulianza kukua, na nyumba nyingi zaidi zikijengwa. Nyumba hizo zilikuwa bado zimejengwa kwa miti na udongo, lakini wakazi walianza kujenga kwa kutumia mawe ya matumbawe pia. Walitumia aina mbili za matumbawe. Kuta zilijengwa kwa kutumia mawe ya matumbawe yaliyochimbwa kutoka ardhini kwa namna ya kifusi, lakini watu walianza kuchukua matumbawe hai kutoka kwenye miamba hiyo pia. Hii iliweza kukatwa kwa urahisi katika maumbo mwororo na mazuri, ambayo walitumia kutengeneza miundo ya kifahari kama matao ya milango. Kipindi hiki msikiti ulijengwa Kilwa. Ulikuwa na mirhabu iliyochongwa upinde kutoka kwa haya matumbawe hai, ambayo bado unaweza kuiona leo kwenye mwisho wa kaskazini wa jengo la Msikiti Mkuu. Msikiti huu ni ushahidi wa kwanza wa Waislamu pale Kilwa. Huenda kulikuwa na jumuiya ya Waislamu hapa awali, ama waongofu mahalia au wageni kutoka ng'ambo, lakini msikiti huo ni ishara ya kwanza ya kudumu kwamba kulikuwa na jumuiya ya Waislamu hapa.






Wakati huo, watu wa Kilwa walianza pia kutajirika zaidi. Walikuwa na mali zaidi, ikiwa ni pamoja na aina mpya za vyombo vya udongo vilivyotengenezwa hapo ikiwemo mabakuli maridadi yaliyopakwa rangi na kupambwa. Ndani ya mji, wafanyakazi walikuwa wakizalisha vitu vya chuma kwa wingi. Chuma kilikuwa kikitengenezwa, pengine kwa ajili ya zana kama majembe

na visu, lakini pia labda kwa ajili ya kuuzwa kwa washirika wa bara na kutoka nchi za kaskazini. Pamoja na chuma, wafanyakazi wa Kilwa walikuwa wakitengeneza vitu kwa shaba, kama vile vijiko, vyombo kama masanduku na vito. Pia walitumia shaba kutengeneza sarafu. Hizi zilitengenezwa Kilwa na zilitumika mjini. Ni ishara dhahiri ya kukua kwa utajiri wa jamii ya Kilwa. Walitengeneza sarafu za shaba, fedha na ikiwezekana dhahabu. Sarafu hizo zimechongwa majina ya watawala wa Kilwa, kuanzia Ali bin al-Hasan, ambaye ndiye mtawala wa kwanza anayetajwa tunayemfahamu kutoka katika mji huo. Hii inaonyesha kuwa baadhi ya watu pale Kilwa hawakuwa tu wakitajirika, bali pia walikuwa na nguvu na watawala walijitokeza miongoni mwao. Makaburi ya Sake huko Kilwa yana makaburi ya matajiri hao wa miaka elfu iliyopita, yenye makaburi yaliyojengwa kwa matumbawe na lipu ya chokaa ambapo watu waliacha sarafu za kuwakumbuka baada ya kufa. Tunashawishika kuwaita watawala hawa 'Masultani', lakini Ali hakutumia jina hilo kwenye sarafu zake na hatujui kama lilikuwa ni jina lililotumika miaka hii ya mwanzo au kama limeongezwa baadaye.

Kadiri Kilwa ilivyokua, inaonekana pia ilijihusisha zaidi na biashara na washirika wa ng'ambo ya bahari. Vitu vilivyoletwa Kilwa vilijumuisha idadi kubwa ya kauri kutoka Ghuba ya Uajemi, na kutoka mbali hadi Uchina. Vingi vilikuwa mabakuli, ambavyo vinatupa taswira ya jinsi maisha ya Kilwa yalivyokuwa yakibadilika, huku kaya tajiri zikila kwa kutumia kauri za Kichina, pengine wakivalia hariri kutoka nje ya nchi pamoja na pamba ya kienyeji. Katika kipindi hiki watu wa Kilwa walianza kuagiza shanga nyingi za kioo, zikitoka India pamoja na Ghuba ya Uajemi. Hizi zingekuwa zinawaliwa na wanawake matajiri, na pengine wanaume, ndani ya mji. Huenda pia zilitumika kama sarafu na kufanyiwa biashara na jumuiya za bara. Shanga za glasi zilisafirishwa kutoka miji kama Kilwa, na kufika mashariki na kusini mashariki mwa Afrika. Shanga nyingi za kioo zinazopatikana katika maeneo kama Zimbabwe zinadhaniwa ziliingia Afrika kupitia Kilwa na kisha kusafirishwa kwa makundi mengine mengi.









Mengi ya majengo unayoyaona leo Kilwa yalijengwa baadaye, kipindi cha karne za 14 na 15 (698 Hijria/1300 BK – 904 Hijria/1500 BK). Mji ulikua sana katika wakati huu. Tunaona hili hasa kwa sababu ujenzi mwingi ulifanyika kwa kutumia matumbawe, badala ya nyumba za udongo za hapo awali. Baadhi ya minara mikubwa zaidi ya Kilwa ilijengwa kipindi hiki. Msikiti Mkuu ulipanuliwa, labda kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya Waislamu. Ilongezewa ukumbi mkubwa wa sala kusini mwa msikiti wa awali, wenye nguzo nzuri na paa yenye kuba.

Kasri la Husuni Kubwa, ambalo ni jengo kubwa kwenye mwamba juu ya bahari upande wa mashariki wa mji mkuu, pia lilijengwa mwanzoni mwa karne ya 14. Jengo hili halifanani na lingine lolote linalopatikana kwingineko kwenye pwani ya Uswahilini. Lina vyumba vingi, baadhi yake pengine yakiwa makazi kwa mmoja wa watawala wa Kilwa na kaya yake.






Moja ya vyumba maarufu sana huko Husuni Kubwa kina bwawa la kuogea la pembenane, ambalo lingelazimika kujazwa na watumishi wanaobeba maji kutoka kisimani, au labda kupanda ngazi kutoka baharini. Ikulu hiyo pia ina sehemu kubwa zinazofikiriwa kuwa za umma zaidi, ikiwemo moja inayojulikana kama 'baraza la hadhira' ambapo inadhaniwa kuwa wageni walitambulishwa kwa sultani. Husuni Kubwa ulikuwa ni mradi mkubwa wa ujenzi, lakini inaonekana haukukamilika na jengo likatelekezwa wakazi walipohama kurudi mjini.



Mji mkuu wa Kilwa pia ulianza kuonekana tofauti sana wakati huu. Badala ya kutumia matumbawe kwa misikiti na makaburipekee, wakazi walianza kutumia matumbawe kujengea nyumba. Mengi ya magofu ambayo unaweza kuona leo katika mji huo yalijengwa katika karne ya 15. Hizi ni pamoja na nyumba zilizo na sifa za kipekee, ambazo zimerithishwa majina baada yake. ‘Nyumba ya Msikiti’ ilikuwa na msikiti wake mdogo ndani kwa ajili ya wenyeji kuswali. ‘Nyumba ya Baraza’ ilikuwa na muundo mzuri wa baraza, ambalo lilijumuisha mabakuli dazeni kadhaa yaliyoingizwa nchini kutoka Ghuba ya Uajemi yaliyopachikwa ndani katika dari. Misikiti kadhaa midogo pia ilijengwa, kama vile ‘Msikiti mdogo wa Kuba’ katikati mwa mji, na Msikiti wa Malindi kaskazini mwa kisiwa hicho.

Nini kilikuwa kikiendelea Kilwa kipindi hicho? Kwa nini kulikuwa na ukuaji huo katika ujenzi? Baadhi ya majibu yanatokana na ukweli kwamba Kilwa ilikuwa imekuwa kituo muhimu cha biashara ya ng’ambo ya nchi. Ilijulikana kama mahali pa kununua dhahabu. Wafanyabiashara kutoka nchi nyingine za Bahari ya Hindi walikuja Kilwa kuchukua dhahabu hiyo na wafanyabiashara wa Kilwa pengine waliibeba katika safari wenyewe. Hii ilimaanisha kuwa kulikuwa na utajiri mwingi katika mji huo na watu walitumia utajiri huo kujenga nyumba nzuri na kufadhili miradi kama vile misikiti. Wafanyabiashara wa Kilwa walikuwa wanazidi kuwa na nguvu. Ikulu iliyopo Husuni Kubwa inatuonyesha utajiri wa kaya moja lakini ikatelekezwa na watu wa mjini wakaanza kujenga nyumba za kifahari. Hii inaonekana kama mabadiliko katika mamlaka, labda kutoka kwa ‘sultani’ au mtawala na kurudi kwa kundi la wafanyabiashara katika mji.





Songo Mnara

Katika kipindi hiki, wakati nyumba kuu zikijengwa Kilwa, baadhi ya watu walianza kujenga katika kisiwa jirani cha Songo Mnara pia. Mji wa Songo Mnara si kama Kilwa, kwa kuwa hauna nyumba za awali, zilizozikwa, chini ya majengo ya matumbawe. Badala yake, mji mzima unaonekana kama ulijengwa haraka sana, mwishoni tu mwa karne ya 14 na mwanzoni mwa karne ya 15 (takriban 791 Hijria/1390 BK – 832 Hijria/1430 BK). Kwa hakika watu waliojenga hapa walitoka Kilwa. Tunaweza kuona kufanana katika baadhi ya majengo, lakini kidokezo kikuu ni katika vitu vyote walivyokuwa navyo. Ufinyanzi wao ulikuwa sawa kabisa na ule ufinyanzi wa kipindi hicho kule Kilwa, walikuwa na vitu vinavyofanana vya chuma na shanga, na walitumia sarafu zilizotengenezwa Kilwa kwa ajili ya kununua vitu mjini. Hatufahamu ni kwa nini baadhi ya wakazi wa Kilwa walihamia Songo Mnara. Labda walihitaji nafasi kubwa zaidi, au walitaka kwenda mbali zaidi na makundi yenye nguvu huko Kilwa? Labda walikuwa na matumaini ya kuanzisha kituo shindani cha biashara kwa ajili ya biashara ya nje? Baadhi ya wanaakiolojia wamependekeza kwamba ilikuwa makazi ya likizo, ambapo familia tajiri za Kilwa walikwenda wakati wa miezi ya joto zaidi.

Hata hivyo, jambo moja tunaloweza kusema kuhusu Songo Mnara, ni kwamba palikuwa mahali pa kidini. Kuna msikiti katikati ya mji, katika uwanja ambao nyumba zote hutazama kuelekea. Kando ya msikiti huo kuna makaburi yenye ukuta kuzunguka. Makaburi, na labda msikiti pia, ndiyo mambo ya awali kabisa kwenye eneo hilo. Kwa hiyo huenda Songo Mnara palikuwa mahali ambapo wenyeji wa Kilwa walizika mababu zao, na kisha wakajenga mji kuzunguka makaburi hayo?




Eneo la kati karibu na msikiti huo iliendelea kuwa mahali pa kuzika wafu. Mamia ya watu walizikwa hapo wakati mji ukikaliwa. Watu waliokuwa wakiishi Songo Mnara waliwakumbuka wale mababu kwa kutoa sadaka kwenye makaburi. Walitandaza matawi ya mitende kwenye makaburi na kula chakula karibu nayo nyakati za ukumbusho. Baadhi ya makaburi kwa hakika yalikuwa ya watu muhimu au watakatifu, na watu walitoa sadaka za sarafu au vitu maalum kama mawe meupe juu ya maziko hayo.

Mara mji wa Songo Mnara ulipojengwa ukawa mahali tajiri na wenye shughuli nyingi. Wakazi waliishi zaidi katika majengo makubwa na mazuri ya matumbawe. Mji mzima umeenea majengo hayo na tofauti na Kilwa kuna nyumba chache sana za udongo kwenye eneo hilo. Uliweza kuingia ndani ya majengo hayo kwa kupanda ngazi pana na kuingia kupitia mlango uliochongwa katika matumbawe hai. Ndani ya mlango ungesafisha miguu yako kwenye jiwe kubwa la duara la matumbawe pale mlangoni. Hii ilikuwa kidogo kama maeneo ya kutawadha katika misikiti wakati huo.



Kisha chumba cha kwanza ambacho ungeingia kilikuwa ua mkubwa wenye ngazi kando kando. Vyumba hivi ni muhimu katika nyumba za Songo Mnara. Kuna vyumba sawa na hivi huko Kilwa na katika miji mingine ya pwani ya Uswahilini vilivyokuwa vya kipindi hiki, lakini Songo Mnara ndiyo mahali penye nyua kubwa na nzuri zaidi.



Ngazi zilijengwa kwa matumbawe na kisha jiwe mchanga lilibandikwa juu ili kutengeneza nyuso ngumu. Huenda watu waliketi kwenye ngazi hizo ili kuzungumza. Tunajua kwamba chakula kililiwa hapa, katika mabakuli maridadi yaliyopakwa rangi na kutengenezwa kienyeji, na katika mabakuli ya kung'ara yaliyokuwa yameingizwa nchini kutoka Uarabuni na Uchina. Chumba kilipambwa kwa uzuri. Kitambaa kingeweza kutundikwa kwenye kuta, ambacho kilipakwa rangi nyeupe kwa kutumia lipu ya chokaa. Viango (zidaka) kwenye kuta vingeweza kutundikiwa taa, maandishi ya Kurani na vitu vya kupendeza. Sakafu ya kati chini ya ngazi ingekuwa imetengenezwa kwa udongo ulioshindiliwa, hasa ukiwa umeletwa ndani ya chumba, ambao ulikuwa rangi nyekundu angavu. Eneo zima lingeweza kuwa la kustaajibisha sana na lingekuwa eneo zuri la kuwaalika wageni na kuwavutia kwa nyumba yako na ukarimu wako.



Kwa upande wa ndani zaidi wa nyumba hizo, wenyeji wa Songo Mnara walikuwa na vyumba vingi vya kulala na vya kuhifadhia bidhaa. Walikuwa na bafu nyingi, zilizokuwa na choo na mitungi mikubwa ya maji na birika ili kuvitunza kwa usafi. Pia walitumia nyumba hizo kwa kazi, kufanya shughuli kama vile kuchakata mazao kutoka mashamba jirani. Jambo moja kuu ambalo watu walifanya katika nyumba ni kwamba walitengeneza uzi wa pamba, wakiusokota na labda kisha kuutumia kutengeneza vitambaa vya nguo na kwa biashara. Kazi hii huenda ilifanywa na wanawake, ambao walikuwa na shughuli nyingi katika maisha ya mji. Tunapata ushahidi wa kazi za wanawake kila mahali mjini, na baadhi ya maeneo yenye vitu vya thamani zaidi yalikuwa pia sehemu ambapo wanawake walifanya kazi. Katika eneo la jiko la nyumba mojawapo, mamia ya sarafu yalipatikana, mahali ambapo wanawake walikuwa wakipika na kutengeneza vitambaa.

Nyumba hizo pasipo shaka zilikuwa muhimu kwa wakazi wa Songo Mnara. Walizijenga kwa kutumia nyenzo zenye nguvu na za kudumu nazo zikawa mahali ambapo waliweka na kuonyesha mali zao walizozithamini sana. Lakini maeneo ya nje ya mji pia yalikuwa muhimu. Jumuiya ya Songo Mnara ilikuwa na misikiti sita. Pamoja na msikiti mkuu uliokuwa katikati ya mji, kulikuwa na msikiti mkubwa wenye kupambwa uliokuwa kaskazini mashariki mwa mji. Huu mara nyingi huitwa 'Msikiti wa Ijumaa' kwa sababu ndio mkubwa zaidi na pengine uliweza kuwaketisha Waislamu wote wa mji huo. Misikiti midogo hupatikana pembezoni mwa mji, haswa kando




ya ufukwe ambapo ingeonekana na mabaharia wanaofika Songo Mnara. Ule uliowaajabu zaidi kati ya hiyo ni msikiti mdogo uitwao 'mnara' (huenda ikimaanisha mnara), ambao uko kwenye kilima kidogo cha matumbawe na umezingirwa na maji wakati wa bahari kupwa.



Wakazi wa Songo Mnara walikuwa wakulima na wavuvi. Walikula samaki na samakigamba wengi, waliopatikana kwenye miamba karibu na kisiwa hicho na pia kwenye maji ya kina kirefu – walijitosa baharini kutafuta samaki wakubwa na pia wanyama kama kobe na nguva. Pia walifuga wanyama. Mbuzi na kondoo walikuwepo kwa wingi katika mji huo. Waliwekwa nje tu ya nyumba, karibu na mlango wa mbele, hivyo nafasi zinazoonekana tupu sana sasa zingekuwa zimejaa uhai na uchafu! Pia walikula ng'ombe, na kutumia maziwa, ingawa hawa walitoka nje ya mji, huenda wakichungwa mahali pengine kwenye kisiwa hicho. Walilima mashamba kote kisiwani, wakiyamwagilia maji kwa kutumia visima ambavyo bado vinaweza kuonekana katika mandhari ya ardhi.

Ndani ya mji, watu walikuwa na shughuli nyingi pia za kutengeneza vitu. Walitengeneza shanga kutoka kwa aina ya ganda inayoitwa aragonaiti, ambayo hutoka kwa chaza mkuu waliomwinua bila shaka kutoka kwa miamba ya matumbawe kwa mkono. Shanga hizo zilitengenezwa katika karakana iliyojengwa kwa kuta za miti na udongo katika eneo la magharibi mwa mji karibu na ufukwe. Mahali hapo pia pangeweza kuwa sehemu ambapo wavuvi walikausha nyavu zao na samaki waliowavua. Kulikuwa na karakana nyingine pia, sehemu ya kundi la nyumba za udongo hapa. Baadhi ni vigumu kuelewa, lakini inaonekana walikuwa wakitengeneza vitambaa na kuvitia rangi, au kutengeneza ngozi kutokana na ngozi za kondoo na mbuzi waliofuga. Sehemu ya kufua vyuma ilionekana mahali hapa, na wahunzi wa chuma wakitengeneza zana za chuma kwa matumizi ndani ya mji.



Pamoja na shughuli hii, Songo Mnara ilikuwa na mahusiano ya kibiashara, sawa na yale ya Kilwa. Kauri zilizong'arishwa kutoka Uajemi, Uarabuni na Uchina zinaonyesha kuwa walikuwa wakikutana na wafanyabiashara wale wale na kufanya biashara sawa na majirani zao huko Kilwa Kisiwani. Walikuwa na shanga za kioo kutoka India, ambazo walizivaa katika maisha yao ya kila siku na pia kufanyia biashara na wengine. Inawezekana walikuwa wakitengeneza shanga za kioo pia, kwa kuchukua baadhi ya zile walizoingiza kutoka India na kutoka China, kisha kuziyeyusha na kuzitengeneza kuwa shanga kubwa zaidi zenye michoro ya rangi nyingi. Moja ya mambo mengine makubwa ambayo Songo Mnara walishiriki na Kilwa ni pesa zao. Walitumia sarafu za Kilwa, zilizotengenezwa kwa shaba, na hizi zilikuwa muhimu katika kununua chakula na vitu mjini. Sarafu zilitumika katika ununuzi wa siku kwa siku. Zilikuwa na majina ya watawala wa Kilwa na hivyo inawezekana kwamba Songo Mnara kwa namna fulani ilitawaliwa na Kilwa. Sarafu hizo hizo pia zinapatikana katika kisiwa cha Mafia, ambacho kilisemekana kutawaliwa na Kilwa.






Historia na Akiolojia

Watu wengi ambao majina yao yameandikwa kwenye sarafu za Kilwa wanajulikana kwetu kutokana na historia. Katika miji mingi ya pwani ya Uswahilini, hadithi zilirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi, zikielezea asili ya mji na hadithi za baadhi ya watawala wa awali. Huko Kilwa, mapokeo haya yanajulikana sana kwa sababu yaliandikwa na Wareno walipofika 909 Hijria/1505 BK, na kuunda hati ambayo kwa kawaida huitwa ‘Kilwa Chronicle’. Matoleo mengine yaliyoandikwa baadaye pia yapo ambayo yanasimulia hadithi kama hiyo.

Mapokeo haya husimulia kisa cha kuanzishwa kwa Kilwa na mfalme wa Kiajemi kutoka Shiraz. Alikuwa mmoja wa ndugu sita aliyesafiri kwa meli kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Mkuu huyu alilipa vitambaa ili kununua kisiwa cha Kilwa kutoka kwa mfalme wa mahali hapo. Hadithi zinatambia kwamba yeye pia alileta Uislamu katika eneo hilo. Mapokeo ya Kilwa pia yanatueleza kuhusu mfululizo wa watawala kule Kilwa. Baadhi yao wanaweza kuendana na mambo mengine tunayojua. Ali bin al-Hasan, kwa mfano, ambaye ametajwa kwenye sarafu nyingi za Kilwa, mara nyingi anahusishwa na Ali wa kwenye hadithi ya asili. Wazao wa mtawala wa kwanza, kulingana na tarihi, walikuwa na mafanikio tofauti. Baadhi yao waliondolewa madarakani, mmoja alikatwa vichwa, na mmoja kutupwa ndani ya kisima.



Hata hivyo, mapokeo pia yanatueleza kwamba Kilwa ilitajirika sana kwa biashara ya dhahabu kati ya Sofala na Ghuba ya Uajemi na ikachukuliwa na nasaba nyingine, Wamahdali, takriban mwaka 698 Hijria/1300 BK. Mtawala mpya wa Kimahdali wa Kilwa, al-Hasan bin Talut, alipanua Msikiti Mkuu kwa ukumbi wa swalawenye kuba. Kisha, wakati wa utawala wa mjukuu wake, al-Hasan bin Sulaiman, kuanzia takriban 718 Hijria/1320 BK, kasri kuu la Husuni Kubwa lilijengwa. Al-Hasan bin Sulaiman alikuwa maarufu. Alijulikana kama Abu al-Mawahib, au “Baba wa Karama”, na aliimarisha uhusiano na Yemen, akajenga misikiti, na akawaalika wanazuoni mashuhuri wa Kiislamu kukaa kwenye kasri lake. Hilo kasri kubwa la vyumba 100, Husuni Kubwa, ndilo kubwa zaidi lililojengwa katika Pwani yote ya Uswahili.


Historia hizi zinatupa maelezo fulani kuhusu baadhi ya watu waliokuwa na nguvu huko Kilwa. Pia tunaelewa hadithi walizosimulia ili kuendeleza nguvu hiyo, ikiwa ni pamoja na kusimulia hadithi za asili yao katika Uajemi au Uarabuni. Zisichoweza kutuambia ni jinsi maisha yalivyokuwa Kilwa na Songo Mnara, au watu wengi wa mjini walifanya nini. Akiolojia imeonyesha wazi kwamba mji ulikua kwa muda kutoka kwa makazi madogo ya wavuvi, na kwamba shughuli zao nyingi na mali zilizalishwa mahali hapo. Wakati wa ukoloni nchini Tanzania, wanahistoria wakati fulani walidai kwamba watu wa Kilwa walikuwa Waarabu, lakini utafiti wa hivi karibuni umeonyesha wazi kuwa jambo hilo si kweli. Ni wazi kwamba karibu wakazi wote wa Kilwa wangekuwa ni Waafrika. Baadhi ya ushahidi bora zaidi kwa hili jambo ni lugha ya Kiswahili yenyewe, ambayo ni lugha ya Kibantu iliyokuzwa kwa karne nyingi katika pwani ya Afrika Mashariki. Maneno ya Kiarabu katika Kiswahili yote ni ya hivi punde sana, yakitoka katika karne chache zilizopita.




Historia za Kilwa zinatueleza kuhusu watu wachache wenye nguvu na hadithi walizotaka kusimulia kuwahusu wao wenyewe. Mengi tunayoyafahamu kuhusu maisha ya Kilwa na Songo Mnara yanatokana na akiolojia. Kumekuwa na utafiti mwingi wa kiakiolojia katika maeneo yote mawili! Akiolojia ni njia ya kujua kuhusu mambo ya kale kwa kutumia vitu na mabaki ya vitu. Watu wa zamani walijenga nyumba, walidondosha takataka, waliacha vitu vimetapakaa huku na huko, na kutapanya mabaki ya vyakula. Pia waliacha vitu kwa makusudi – dhahiri zaidi kati ya haya ni maziko ya watu, makaburi yaliyojengwa ili kuwakumbuka na vitu vilivyoachwa kwenye makaburi hayo. Majengo hayo, vitu na takataka bado vinaweza kuwepo, hata mamia ya miaka baadaye. Vitu vya zamani zaidi huzikwa chini ya vilivyo vipya zaidi, na kutengeneza tabaka za takataka na mabaki. Wanaakiolojia hutafuta mabaki hayo, na kuchimba chini kupitia tabaka mpya zaidi za takataka na ardhi ambayo imejijenga hadi kufikia vitu vya awali vilivyo chini.

Huko Kilwa Kisiwani, akiolojia ya kwanza ilifanywa na Mwingereza aitwaye Neville Chittick. Alikuwa Mkurugenzi wa Tanganyika wa Mambo ya Kale alipoanza kazi pale Kilwa miaka ya 1960. Baada ya Tanzania kupata uhuru kutoka kwa Uingereza, Chittick aliamia kuwa mtafiti wa kudumu katika Taasisi ya Uingereza ya Afrika Mashariki, yenye makao yake nchini Kenya. Aliendelea kufanya kazi pale Kilwa na akachapisha taarifa za uchimbaji wake katika kitabu cha mwaka 1974.

Uchimbaji wa Chittick haukuwa tu wa kwanza huko Kilwa, ulikuwa ni baadhi ya uchimbaji wa kwanza kwenye pwani ya Afrika Mashariki na alikuwa na nia kubwa ya kujaribu kujua magofu yalikuwa ya miaka mingapi, na ni nani aliyeishi huko. Hii ilimaanisha zaidi kwamba alisafisha majengo. Chittick alipofika Kilwa majengo mengi makubwa ya zamani yalikuwa yamezikwa. Uliweza tu kuona vilele vya kuta za Husuni Kubwa, kwa mfano, kwa sababu ardhi ilikuwa imejengeka pande zote kuizunguka. Chittick alikuwa na timu ya wafanyakazi mahalia, wanaume na wanawake ambao walifanya kazi kwa bidii kusafisha kiasi kikubwa cha ardhi. Walichimba chini hadi kwenye sakafu ya Husuni Kubwa, pamoja na kuusafisha Msikiti Mkuu, misikiti midogo na nyumba kubwa kadhaa za mawe.





Katika eneo linalozunguka baadhi ya nyumba hizi leo bado unaweza kuona jinsi zinavyokaa kwenye bonde dogo ardhini – hii ni kwa sababu ardhi iliyozizunguka iliondolewa.

Pamoja na kusafisha nyumba hizo, Chittick alitilia maanani sana vitu vilivyokuwa ndani ya nyumba. Alihesabu, kurekodi na kuandika juu ya aina nyingi tofauti za ushahidi, lakini shauku yake kubwa ilikuwa vyombo vya udongo vilivyoingizwa kutoka nje ya nchi. Kulikuwa na sababu mbili kwa hili. Kwanza, Chittick alikuwa akijaribu kufahamu umri wa magofu huko Kilwa, na vyombo vya udongo vilivyoingizwa kutoka nje tayari vilikuwa vikijulikana kutoka sehemu kama vile Iran na hivyo alijua takriban umri wake. Pili, Chittick aliamini kuwa Kilwa ni mji uliojengwa na Waarabu waliokuja katika pwani ya Afrika. Hakuwa na shauku sana na vitu vya ‘Kiafrika’ kama vile ufinyanzi mahalia, ingawa kwa bahati kwetu alivirekodi!

Uchimbaji wa Chittick ulionyesha kuwa Kilwa Kisiwani ulikuwa mji wa zamani sana. Alichimba chini ya sakafu za nyumba na alikuwa mtu wa kwanza kuona nyumba za udongo kutoka karne ya 9. Alielezea historia ndefu ya mji huo, kutoka kwa makazi haya yaliyojengwa kwa nyumba za udongo hadi mji mkuu wa biashara kutoka karne ya 11 na kuendelea. Pia alitumia vitu vilivyopatikana katika mji huo kufikiria jinsi maisha yalivyokuwa hapa zamani. Alijikita zaidi kwenye kauri zilizoagizwa kutoka nje ya nchi na pia shanga za kioo, akijadili jinsi Kilwa ilivyokuwa bandari ya kimataifa na kuonyesha uhusiano huo na vitu kutoka nje ya nchi. Moja ya sehemu alizotumia muda mwingi ni kutaka kuelewa sarafu zilizozalishwa Kilwa, akijaribu kuzihusianisha na watawala waliotajwa katika kitabu cha Tarihi ya Kilwa.

Hivi sasa aina ya uchimbaji uliofanywa na Chittick ni wa kizamani. Wanaakiolojia katika Afrika mashariki wamebadili nia zao na kufikiria zaidi maisha yalivyokuwa, badala ya kubaini tu tarehe na uhusiano wa kibiashara. Huko Kilwa kumekuwa na ufuatiliaji wa miradi ya mwanaakiolojia anayeitwa Profesa Felix Chami, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Moja ya mambo muhimu aliyoyafanya Chami ni kuchunguza baadhi ya maeneo ya mjini nje ya majengo ya matumbawe. Alifahamisha kuwa eneo liitwalo Nguruni, karibu na Husuni Kubwa, halina majengo bali lina takataka nyingi za kale zitokanazo na uzalishaji wa chuma. Alifikiria eneo hili kuwa mahali ambapo chuma kilikuwa kikitengenezwa kwa kiwango kikubwa. Fikra za namna hii, ambazo hufikiri Kilwa kuwa mji ambao watu waliishi na kutengeneza vitu, ni njia tofauti kabisa ya kufikiria maisha ya mjini hapo.






Hivi karibuni, uchimbaji wa Songo Mnara wa Profesa Jeffrey Fleisher na Profesa Stephanie Wynne-Jones umebadili njia ambazo tunaweza kuifikiria Kilwa zaidi. Kazi yao pale Songo Mnara ilitumia mbinu mpya za kiakiolojia ili waweze kufanya zaidi ya kuchimba tu chini na kujua nini kilikuwa chini ya nyumba hizo. Kwa mfano, waliipima ardhi katika eneo lote na kuangalia kemia yake. Hii ilimaanisha kwamba wangeweza kuona mahali ambapo wanyama walikuwa wamehifadhiwa zamani, nje ya nyumba kubwa, kwa sababu kinyesi cha wanyama kilikuwa kimebadilisha kemia ya udongo. Pia walitumia mbinu kama vile uchunguzi wa kijiofizikia, kwa kutumia mashine kuchanganua eneo lile lote na kupata mabaki yaliyozikwa kama sehemu za uhunzi wa chuma, au nyumba za udongo ambazo hazikuonekana tena kwenye uso wa ardhi.

Fleisher na Wynne-Jones pia walichimba sana katika mji wa Songo Mnara. Tofauti na Chittick, wao walirekodi kila kitu ardhini, wakichora ramani ya takataka zilizotupwa na wakazi wa Songo Mnara katika maeneo yote tofauti tofauti. Hii ilimaanisha kwamba wana uwezo wa kuzungumzia kile watu walifanya katika majengo na maeneo tofauti. Ni kutokana na kazi hii tunaweza kuona kwamba watu walikaa katika nyumba za matumbawe na kutengeneza vitambaa kwa uzi wa pamba. Tunajua kwamba wanawake walikusanyika kwenye kisima katikati ya mji, ambapo pia mara nyingi walipoteza baadhi ya shanga zao, au kuvunja mitungi waliyokuwa wamebeba. Tunaweza kuona sadaka zikiwekwa kwenye makaburi katikati ya eneo hilo, na maeneo ambayo wanyama walifungiwa. Fleisher na Wynne-Jones pia walitumia muda mwingi kufikiria takataka zilizoachwa na wakazi wa Songo Mnara. Walirekodi na kutambua kila mfupa wa mnyama, kwa hivyo tunajua walichokula, na hata kila mtama uliochomwa au nafaka ya mchele. Kwa kurekodi kila kitu na kufikiria mahali ambapo kila aina tofauti ya kitu kilikuwa, kwa kuzingatia kila chombo, cha kienyeji na cha kigeni, wametoa taswira ya thamani zaidi ya maisha katika miji. Mengi ya yaliyoandikwa hapo juu yanatokana na kazi hii.








Ureno, Omani na karne za baadaye

Mnamo 909 Hijria/1505 BK, mashua ya askari wa Kireno ilifika Kilwa. Katika kipindi hiki Wareno walikuwa wamepata njia ya kuzunguka kusini mwa Afrika, nao walikuwa wakisafiri mwelekeo wa juu wa pwani kutoka kusini hadi kaskazini. Walitaka kutawala biashara katika Bahari ya Hindi. Walivutiwa hasa na dhahabu kutoka kusini mwa Afrika na viungo kutoka India. Ingawa Kilwa yenyewe haikuwa na dhahabu, mji huo ulikuwa bandari kuu ya biashara ya dhahabu kutoka kusini mwa Afrika. Wareno walianza kuchukua dhahabu kutoka Msumbiji moja kwa moja, na kupunguza usambazaji wake Kilwa. Pia waliamua kuharibu nguvu za Kilwa na wakarudi kuushambulia mji. Waliweka boma ya askari pale Kilwa. Kulikuwa na askari 12 tu, lakini walikuwa na bunduki, na pia walikuwa na jeshi zima la wanamaji la Ureno nyuma yao!




Wareno walijenga ngome huko Kilwa, iitwayo Gereza, ambayo kwa Kireno ina maana ya kanisa lakini kwa Kiswahili imekuja kumaanisha kifungo. Hii inatupa vidokezo kuhusu jinsi watu wa eneo hilo walipata uzoefu wa makazi ya Wareno.

Kilwa ilifia haraka wakati huu. Wareno walikuwa na vurugu kali katika kutwaa mamlaka, lakini kuna uwezekano kwamba sababu kubwa ilikuwa kupotea kwa udhibiti wa kiuchumi kwa watu katika mji huo. Hawakuweza tena kufanya biashara ya dhahabu, na inawezekana kwamba maisha ya mjini yakawa magumu. Inaonekana kwamba watu wengi waliondoka tu mjini katika kipindi hiki. Nyumba zilitelezwa na nyingi zilianguka na hazikutengenezwa.

Kidokezo kingine cha kuachwa kwa Kilwa kwa wakati huu kinatokana na akiolojia pale Songo Mnara. Hapa mji ulitelezwa kabisa na inaonekana haukukaliwa tena. Uchimbaji katika eneo hilo umeonyesha kuwa kulikuwa na mazishi mengi wakati huu, ikiwemo pia mazishi ya watoto. Haiwezekani kuonyesha hili kwa kuangalia makaburi, lakini inawezekana kuwa Wareno walikuja na ugonjwa kama ndui huko Kilwa, na kwamba hii ikasababisha kutelezwa kwa miji ya Kilwa na Songo Mnara.

Mnamo 1108 Hijria/1698 BK Wareno walishindwa vita vya muda mrefu dhidi ya vikosi vya Omani pale Fort Jesus huko Mombasa, Kenya. Punde Waomani walichukua makoloni mengi ya Wareno maeneo ya pwani. Pale Kilwa, walipanua Gereza na kuifanya ngome kubwa zaidi. Jengo hilo leo lina mwonekano wa Kiomani zaidi kuliko wa Kireno.



Wakati wa ukoloni wa Kioman katika karne ya 19, walikwenda hatua moja zaidi ya Wareno na wakajenga bandari mpya, pwani ya juu zaidi katika mahali paitwapo Kilwa Kivinje.

Bandari ya Kilwa Kisiwani sasa haikuwa tena kituo ilichokuwa. Ilikuwa imenyang'anywa mamlaka na mahusiano ya kibiashara, na watu walikuwa wametawanyika, huenda kutokana na magonjwa. Lakini katika karne ya 18 mji ulipata fursa mmoja zaidi ya utajiri, wakati mtawala wa Kilwa aliposaini mkataba wa kusambaza watumwa kwa makoloni ya Wafaransa huko Reunion na Mauritius. Katika kipindi hiki, Kilwa ilitajirika tena kwa muda mfupi, japo majengo na mji ulikuwa tofauti sana. Watawala wa wakati huo walijenga boma kubwa la ukuta ambalo sasa linaitwa 'Makutani', pamoja na kasri kubwa la wale waliotajirika kutokana na biashara hiyo. Nyumba kubwa za mawe za karne za awali hazikujengwa upya wala kuishi watu, kwa hiyo inawezekana ni vikundi vichache tu pale Kilwa vilivyokuwa vinatajirika wakati huu.

Hata hivyo, hadithi ya Kilwa haijaisha. Watu wanaoishi katika visiwa vya Kilwa na Songo Mnara ndio warithi wa hadithi hii ndefu. Wao ni Waislamu, na wanaweza kufuatilia dini hiyo kupitia ukoo wao hadi kwenye baadhi ya karne za mwanzo kabisa za Uislamu. Wanatunza na kusimulia hadithi za watawala na wakazi wa zamani. Nao ndiyo sura ya hivi punde zaidi katika hadithi ya Kilwa, jumuiya ya visiwani yenye msingi wa rasilimali na fursa za kienyeji, wakipokea mageuzi



ya hali ya kimataifa inayobadilika. Leo, utalii wa Urithi wa Dunia ni sehemu muhimu ya uchumi wa Kilwa na hii inapaswa kuhusisha jamii mahalia kadri zinavyoendelea kutumia hizo rasilimali mahalia katika kuunda ulimwengu wa WaSwahili leo.